*Kioo cha Lugha, Juz. 23(1), 67-85*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i1.5

# Mikinzano ya Kimtazamo baina ya Wahusika Inavyobainisha Falsafa ya Kiafrika: Mifano kutoka Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007)

*Winne S. Mtega*[1]

## Ikisiri

Tofauti za kimtazamo baina ya wahusika zimekuwa zikijitokeza katika kazi mbalimbali za riwaya. Watunzi wa kazi hizo wamekuwa na kawaida ya kuwavisha wahusika uhusika unaopambanua mawazo, imani, itikadi na falsafa mbalimbali zinazoongoza maisha yao. Kuwapo kwa mitazamo hiyo, kumechochea tafiti nyingi kuchunguza falsafa ya waandishi wa kazi hizo, mitazamo ya wahusika na uhusika wao na Uafrikanishaji wa kazi hizo, hususani za riwaya. Makala hii inalenga kuchunguza mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika na namna inavyobainisha falsafa ya Kiafrika. Data za utafiti zimepatikana uwandani kupitia njia ya usomaji na uchambuzi matini. Mchakato wa uchambuzi umeongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) imejitokeza katika masuala ya ndoa, uzazi, malezi, utamaduni na ujamaa. Vipengele hivyo ndivyo vimeibua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika na kubainisha falsafa ya Kiafrika kwamba maisha ya Mwafrika yamejengwa katika kuthamini uzazi kama mhimili wa kuwapo na mwendelezo hai wa vizazi.

## 1.0 Utangulizi

Uhai wa simulizi la kifasihi hujengwa na wahusika ambao mtunzi huwatumia kuwasilisha maudhui lengwa. Mtunzi huwajenga wahusika kiubunifu kwa kuwavisha imani, itikadi na mitazamo mbalimbali ambayo huwapambanua na kuwatofautisha. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi (Senkoro, 1983; Wamitila, 2002). Katika mtazamo wa kihalisia, viumbe hawa huakisi hali halisi katika ulimwengu wa binadamu, ingawaje uhalisia unaorejelewa hapa si wa moja kwa moja. Kwa mujibu wa Hawthorn (2010), wahusika hubadilika kulingana na masuala yanayomkumba binadamu katika ulimwengu halisi. Mabadiliko hayo husababishwa na ukweli kwamba wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira na malengo ya mtunzi wa kazi husika. Hivyo, wasanii kama sehemu ya jamii huunda kazi ya sanaa kulingana na uhusiano wao na jamii. Hii

[1] Mhadhiri, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu, Mkwawa, Iringa, Tanzania. Baruapepe: mtegawinnie19@gmail.com

inamaanisha kwamba kazi za fasihi haziibuki katika ombwe bali zinachimbuka kutokana na mifumo anuwai ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii (Innes, 1974; Mutembei, 2000; Samwel, 2015; Mulokozi, 2017).

Kiutamaduni, jamii zinafungamana na falsafa ya jamii inayojumuisha mfumo mzima wa maisha ya jamii, mila, desturi na imani zinazoongoza maisha ya Waafrika (Mbiti, 1990; Makumba, 2005). Kwa muktadha huo, ni dhahiri kwamba mitazamo ya wahusika wa kazi za fasihi hujengwa katika namna ambayo hupambanua na kubainisha falsafa zilizopo katika jamii lengwa ya mtunzi. Hivyo, ubunifu wa kazi ya fasihi humwezesha msanii kumfinyanga na kumuumba mhusika kiakili, kimwili, kinafsi, kiitikadi na kimtazamo. Wahusika hao hujengwa kwa namna ambayo huweza kutofautiana kimawazo na kimtazamo. Tofauti za kimtazamo baina ya wahusika huwepo ili kupambanua maudhui, kuendeleza visa na vitushi vya simulizi husika, kupambanua falsafa fulani wanayofungamana nayo na kukamilisha kusudi la mtunzi. Kwa kuzingatia hilo, katika makala hii wahusika ni dhana muhimu inayotusaidia kuonesha namna mikinzano yao ya kimtazamo inavyobainisha falsafa ya Kiafrika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*.

Dhana ya mtazamo ni telezi na ngumu kuitolea maelezo mwafaka. Kimsingi, mtazamo unahusu mahusiano kati ya binadamu, sifa za kisaikolojia na namna mambo yanavyoonekana kwetu. Kulingana na Rimmon-Kenan (1983), mtazamo ni namna hadithi inavyoweza kupewa maana, yaani ni yale mambo yanayotuwezesha kuumba maana kutokana na namna msimulizi wa hadithi anavyoyaweka matukio yake anayoyasimulia. Naye Roberts (1995) anasema kwamba, mtazamo ni msimamo wa msimulizi wa hadithi ambao waandishi huutumia katika kazi zao za kisanaa. Kwa mantiki hiyo, mtazamo ni zile maana, ujumbe, msimamo au falsafa ya mtunzi wa kazi ya fasihi kuhusu masuala mbalimbali katika maisha ya binadamu. Mtazamo unahusu masuala kadhaa ambayo mtunzi amedhamiria kuyapitisha kwa hadhira yake. Mtazamo unaweza kuwa wa kuunga mkono jambo fulani, kutofautiana au kukinzana juu ya jambo fulani. Mtazamo wa wahusika huwasilishwa kupitia sauti-neni au msimulizi katika hadithi. Ndani ya mtazamo ndimo kuna dhamira na ujumbe wa mwandishi na namna anavyoyaona masuala kadha wa kadha yanayojadiliwa katika kazi husika ya fasihi. Aina mbili kuu za mtazamo ni mtazamo wa ndani, ambao huwakilishwa na mhusika aliye ndani ya hadithi husika, na mtazamo wa nje, ambao huwakilishwa na sauti iliyo nje ya hadithi husika (Wamitila, 2002). Ndani ya aina hizi za mtazamo kuna mianda (aina ndogo) au tofauti za mitazamo ambapo kuna mwanda wa kisaikolojia, mwanda wakati, mwanda wa kiisimu, mwanda wa kiitikadi na wa kifalsafa (Uspensky, 1973; Prince, 1982; Simpson, 1983; Jahn, 2005). Kwa kuzingatia aina hizo, makala hii inamakinikia mtazamo wa nje na ule wa ndani katika kufafanua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika inavyobainisha falsafa ya Kiafrika katika riwaya teule.

Kezilahabi (1985) anaeleza kuwa falsafa ya Kiafrika ni zao la tafakuri tunduizi ya umma wa Kiafrika katika mazingira yao. Tafakuri hiyo hujipambanua

kupitia misingi ya tamaduni, imani, itikadi, mitazamo na maarifa waliyonayo juu ya maisha na mazingira yao. Mtazamo wa Kezilahabi unabainisha kuwa Waafrika wana falsafa yao ambayo imefungwa katika namna wanavyoyapambanua mazingira yao. Naye Mihanjo (2006) anaeleza kuwa ni vigumu kueleza falsafa ya Waafrika ni ipi kutokana na ukweli kuwa bara la Afrika lina mwingiliano wa tamaduni mbalimbali. Kwa sababu hiyo, ni vigumu kuwa na mawazo jumuifu ya kifalsafa yanayowajumuisha Waafrika wote katika muktadha wa kijiografia. Ugumu unaoelezwa na Mihanjo juu ya kuielezea falsafa ya Kiafrika unapambanuliwa na Ngugi (1996) na Mihanjo (2007) kupitia mawazo yanayoshabihiana kuwa falsafa ya kweli ya Waafrika inaweza kutambuliwa kupitia utamaduni wao ambao hujumuisha lugha, mila na desturi za jamii hizo.

Aidha, Mutembei (2014) na Chuachua (2016) wanaeleza kuwa falsafa ya Kiafrika ni miongozo inayowakilisha tajiriba, mawazo na mitazamo ya Waafrika wenyewe ambayo hupatikana kwenye vyanzo vya kihistoria, maandishi ya kitaaluma na ya kifasihi pamoja na masimulizi ya kale na ya sasa. Falsafa hiyo huelezea tamaduni, historia na mambo mbalimbali yanayowapambanua na kuwaunganisha Waafrika. Mtazamo huu unaonesha kuwa Waafrika wana mambo yao yanayowatambulisha na kuwaunganisha wenyewe kama Waafrika. Mulokozi (2017) anahitimisha kuwa wataalamu wengi wanakubaliana kuwa falsafa ya Kiafrika ipo na hutolewa kwa kinywa kwa njia ya mijadala, masimulizi, misemo, sanaa, nyimbo na visasili, na kushadidiwa na mila na miviga kama ibada na matambiko. Wataalamu mbalimbali wa fasihi na falsafa ya Kiafrika kama Tempels (1959), Mbiti (1990), Alembi (2001) na Mulokozi (2017) wanakubaliana kuwa falsafa ya Kiafrika ina vijenzi vyake ambavyo huifinyanga, huibainisha na kuitofautisha. Vijenzi hivyo ni kuwapo kwa imani, itikadi na maarifa asilia kuhusu uzazi, dhana ya uduara, itikadi ya kani, matumizi ya rangi, kifo na uhai, sihiri na uganga, umoja na ushirikiano, kuheshimu miungu na wahenga, kuheshimiana na kuheshimu maadili ya jamii na wakati. Kwa hiyo, mitazamo ya wataalamu hao inatuondolea utata juu ya kuielezea falsafa ya Kiafrika, hivyo, kutuachia nafasi ya kuifasili falsafa ya Kiafrika kuwa ni imani, mitazamo, itikadi na miongozo iliyobeba mawazo, maarifa na tamaduni za Waafrika, ambazo hupatikana katika maandishi ya kitaaluma na kifasihi, masimulizi ya kihistoria na katika sanaa zao. Kwa kuzingatia fasili hiyo, makala hii imemakinikia kufafanua mikinzano ya kimatazamo baina ya wahusika inavyobainisha falsafa ya Kiafrika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007).

Kwa upande wa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, kuna tahakiki mbalimbali zimefanywa na wahakiki wengi wa fasihi ambao kila mmoja amejiegemeza katika mielekeo na malengo mahususi ya uhakiki wake. Miongoni mwa wahakiki hao ni Senkoro (1983, 2011), Mulokozi (1983), Mlacha (1991), Wamitila (1997), Wafula (2002), Diegner (2005) na Ilomo (2017). Kwa mfano, Mulokozi (1983) na Senkoro (2011) wanahakiki kipengele cha maudhui katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na kueleza kuwa riwaya hiyo inashughulikia

mivutano mbalimbali ya kijamii, kiitikadi, kifalsafa na kiuchumi inayojitokeza sana katika jamii ya Kitanzania. Mulokozi anabainisha mivutano hiyo kwa kuiweka katika viwango viwili ambavyo ni kiwango cha ubinafsi na cha kijamii huku akionesha wazi upana wa tatizo kwa namna lilivyojitokeza katika riwaya husika. Aidha, Wamitila (1997) anadai kuwa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ni mfano bora wa motifu ya dunia kama mahali pabaya pa kuishi na kuwa kuanzia mwanzo mwandishi anachora picha ya ulimwengu ulio duni na usioaminika. Anaonesha namna uwanja huu wa dunia ulivyobeba mambo mabaya na ya hatari katika maisha kama vile usaliti, ukatili, wizi, na imani za kishirikina. Ilomo (2017) amechunguza mbinu za ujenzi wa wahusika na usawiri wa sifa zao katika *Dunia Uwanja wa Fujo*. Ilomo anaonesha uhusika wa wahusika wa riwaya hiyo na namna walivyouvaa uhusika wao kupitia kauli na matendo yao. Kwa jumla, tunapoangazia tafiti na tahakiki nyingi kuhusu riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, tunabaini kwamba kuna haja ya kuchunguza namna mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika inavyoweza kubainisha falsafa ya Kiafrika. Kufanya hivyo, kutasaidia kufahamu namna waandishi wa kazi za fasihi wanavyojenga wahusika wanaobainisha imani, maarifa, hulka zinazompambanua Mwafrika na falsafa inayomwongoza.

## 2.0 Muhtasari wa Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*

*Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) ni riwaya iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Riwaya hii imegawanyika katika sehemu tatu, huku kila sehemu ikiwa imegawanyika katika sura mbalimbali. Sehemu ya kwanza ya riwaya hii inaelezea historia ya makuzi ya mhusika mkuu na maisha ya wanakijiji wa Bugolola. Katika sehemu hii tunasimuliwa kuwa maisha ya wanakijiji hao yalitawaliwa na umoja na ushirikiano, imani za sihiri na ushirikina, visasi, ulevi. Aidha, mwandishi anasimuliwa namna mhusika mkuu, Tumaini, alivyokua kwa kuchukiwa pale kijijini kutokana na tabia zake. Sehemu ya pili inahusu safari ya Tumaini, Anastazia na John ambaye ni rafiki wa Tumaini kuelekea Mwanza, na uamuzi wa Tumaini kuelekea Dar es Salaam baada ya kutopapenda Mwanza. Tunaelezwa kuwa safari yao iliishia Shinyanga baada ya kuamua kuishi huko. Sehemu ya tatu inahusu kutangazwa kwa Azimio la Arusha na athari zake kwa wananchi. Sehemu hii inaeleza kuwa katikati ya mafanikio ya wananchi, akiwamo Tumaini, Azimio la Arusha lililohubiri siasa ya Ujamaa na Kujitegemea lilitangazwa na hivyo kusababisha machafuko kutokana na kutaifishwa kwa mashamba ya watu, akiwamo Tumaini. Hali hii ilimkatisha tamaa Tumaini ambaye aliamua kumuua Mkuu wa Wilaya, tukio lililosababisha Tumaini kukamatwa na kuhukumiwa kunyongwa. Masimulizi ya riwaya hii kwa kiasi kikubwa yamejikita katika kueleza maisha ya mhusika Tumaini, tangu akiwa mtoto mpaka kifo chake. Mwandishi ametumia wahusika wengine wengi katika simulizi ili kuujenga na kuukamilisha uhusika wa Tumaini.

## 3.0 Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika

Ontolojia ya Kiafrika ni nadharia iliyoasisiwa na Placide Temples katika kitabu chake kinachojulikana kama *Bantu Philosophy* (1959). Temples anaeleza kuwa, Ontolojia ya Kiafrika inafungamana na kani uhai ambayo huhusishwa na Mungu, uungu, mwanadamu na jamii. Kani uhai hiyo ndiyo huongoza maisha ya mwanadamu, huyaimarisha na hata kuyadhoofisha. Baadhi ya Waafrika walioendeleza nadharia hii ni Kagame (1956), Mbiti (1975), Kezilahabi (1985), Mihanjo (2004) na Mulokozi (2017). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inajumuisha misingi kama vile dini, uanthropomofia[2], familia pana ambayo hujumuisha waishio sasa, waliofariki na ambao hawajazaliwa; ulimwengu wenye nyuga tatu[3], uyakinifu wa kipragmatiki[4], ujamiishaji wa kiduara[5], mtazamo wa umosi[6], kuthamini sana uzazi, imani katika sihiri na uchawi, miungu wengi, dhana ya wakati, kuthamini kazi, itikadi ya kani, kuheshimu wahenga na mahoka, jaala badilifu, umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo. Misingi iliyotajwa ndiyo malighafi ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Mulokozi anaongeza kuwa misingi hiyo inapochukuliwa pamoja na miviga, visasili na masimulizi ndiyo hutupa falsafa ya Kiafrika, yaani majumuisho ya tafakuri kuhusu kuwapo kwao, maisha yao na hatima yao. Hii ni falsafa ya kijadi ya Kiafrika ambayo inatofautiana katika baadhi ya mambo na ile ya kigeni lakini inayokaribiana sana na uyakinifu[7]. Mtazamo huu unaonesha wazi ufaafu wa Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika katika kufanikisha lengo la makala hii la kupambanua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika inavyobainisha falsafa ya Kiafrika katika riwaya teule. Makala hii imetumia baadhi ya misingi ya nadharia hiyo kama: kuthamini uzazi, umoja, mshikamano na ukamilishano wa maumbile, itikadi ya kani ambayo huhusisha miiko na laana, heshima na kuheshimiana na nguvu za kauli.

---

[2] Kumtanguliza binadamu; imani, miviga, mzunguko wa kuwapo na kuwa hapahapa duniani (Mulokozi, 2017).

[3] Ardhi (duniani) wanamoishi watu, mazimwi na viumbe wengine, kuzimu wanakoishi mizimu na wahenga pamoja na juu au mbinguni wanakoishi Mungu na miungu (Mulokozi, 2017).

[4] Mtazamo wa kujali zaidi hali na mahitaji ya sasa (kuliko yaliyopita au yajayo) na kujali vitendo kuliko nadharia (Mulokozi, 2017).

[5] Kuzaliwa, kuota meno, unyago, kuoa/kuolewa, uzee, kufariki, kuwa mzimu na kuzaliwa tena (Mulokozi, 2017).

[6] Mtu ni zao na sehemu ya mazingira yake; kwamba mwili na roho havitenganishwi na havitenganiki isipokuwa baada ya mauti; kwamba kila kitu katika mazingira kimebeba kani-uhai na inabidi kiheshimiwe na kuthaminiwa (Mulokozi, 2017).

[7] Mtazamo wa uyakinifu ni ule usioutukuza ukale wa Kiafrika uliopitwa na wakati bali huchunguza Waafrika wa leo kwa kuzingatia kuwapo kwao, harakati zao za sasa za maisha, siasa na tabaka. Mtazamo huu haupuuzi mabadiliko ya jamii, miingiliano na harakati za maisha za sasa katika kuipambanua falsafa ya Kiafrika (Mulokozi, 2017).

## 4.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za utafiti huu zilipatikana maktabani. Mbinu ya usomaji na uchambuzi matini ilitumika ili kupata data msingi katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007). Matini teule ilisomwa kisha uchambuzi ulifanyika. Uchambuzi uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika huku ukiegemezwa katika kufafanua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika inavyobainisha falsafa ya Kiafrika katika riwaya teule. Riwaya hii iliteuliwa kutokana na upekee na ubunifu wa mtunzi katika kuwajengea wahusika wake uhusika uliobeba mitazamo inayopambanua falsafa zinazowaongoza.

## 5.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inajadili mikinzano ya kimtazamo baina wahusika inavyobainisha falsafa ya Kiafrika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Vipengele vilivyojadiliwa ni ndoa, uzazi, malezi, utamaduni na ujamaa.

### 5.1 Ndoa

Hiki ni kipengele kimojawapo kinachojitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Mwandishi anaonesha mikinzano ya kimtazamo juu ya suala la ndoa kupitia namna anavyowajengea uhusika wahusika wake na kuonesha jinsi mitazamo juu ya ndoa inavyobainisha falsafa ya Kiafrika. Mwandishi anawatumia wahusika Mama Resi na Tumaini kuonesha mkinzano wa kimtazamo juu ya suala la ndoa. Anaonesha namna Mama Resi anavyoitazama ndoa kama asasi inayojengwa katika misingi ya haki na usawa, uwajibikaji na ushirikishwaji baina ya mwanamume na mwanamke. Mtazamo huo unakinzana na wa Tumaini ambaye anaitazama ndoa kama asasi inayojengwa katika upendo, heshima na kuheshimiana. Mwandishi anadhihirisha haya kupitia majibizano ya wahusika wake kama ifuatavyo:

> Inakwendaje hata ukaoa msichana ambaye hakusoma?
>
> "Ni mapenzi tu, Mama Resi"
>
> "Mapenzi gani hayo! Mimi ninafahamu kwa nini umemwoa. Umemwoa ili uweze kumwonea. Unataka mwanamke ambaye unaweza kumuamrisha kama mtoto mdogo, karibu kama mtumwa? "Kwa nini unasema hivyo?" Nimesema vile kwa sababu ninaamini katika usawa kati ya bwana na mke. Watu waliosoma wanapenda kuoa wasichana ambao hawana elimu ya juu kwa sababu hii. Wale wenye elimu wataolewa na nani? (uk. 71).

Katika nukuu hii Mama Resi anaonesha mtazamo juu ya tofauti za usawa katika ndoa zinazojitokeza kati ya kuoa mwanamke aliyesoma na asiyesoma. Anaamini kuwa mwanamume huoa mwanamke ambaye hajasoma ili amfanye mtumwa. Hivyo, anamtazama Tumaini kama kijana mkosefu ambaye ananyang'anya uhuru wa wasichana ambao hawajaenda shule ili awafanye watumwa wake. Mtazamo wa Mama Resi unakinzana na wa Tumaini ambaye anaamini kuwa amemwoa

Anastazia kutokana na upendo. Mwandishi anaonesha mtazamo wa Tumaini juu ya kuwapo kwa usawa katika ndoa kupitia namna Tumaini anavyohoji juu ya kuwapo kwa usawa baina yake Mama Resi na mumewe Denis. Mwandishi anabainisha hilo anaposema:

> Wewe na Dennis mko sawa?” “Mimi na bwana wangu tunaamini katika jambo la usawa. Hata mimi ninaweza kutoa maoni yangu mbele ya bwana wangu. Denis anafahamu sana kupika, tunapeana zamu, mara nyingi tunabishana mezani. Unacheka! Si jambo la ajabu. Katika jamii za Kizungu utakuta mara nyingi mwanamke ndiye ana sauti zaidi kuliko bwana.” Mama Resi, jambo la usawa linakuharibu mawazo yako bure. Jambo la maana katika jamii yoyote ile ni heshima. Bwana mke, hata kama wanajidai kwamba wao ni sawa, wasipopeana heshima jamii yao haitakuwa thabiti kamwe…” (uk. 71).

Nukuu inaonesha kuwa mtazamo wa Tumaini juu ya usawa katika ndoa unakinzana na wa mama Resi. Tumaini anaamini kuwa mtazamo wa mama Resi umejengwa katika imani ya Kizungu ambayo inatazama misingi ya ndoa kuwa ni usawa, uhuru wa kimawazo, kimaamuzi, mgawanyo wa majukumu na ushirikishwaji baina ya mume na mke na mke kupewa nafasi ya kushauri na kuhusika katika mazungumzo muhimu. Mtazamo huu unakinzana na wa Tumaini ambaye analitazama suala la haki na usawa kama jambo lililopotoshwa na linalokengeusha desturi za Kiafrika. Tumaini anaamini kuwa ndoa inajengwa katika misingi ya upendo na kuheshimiana baina ya mke na mume. Mtazamo wa Tumaini unapambanua usawa wa Kiafrika ambao unajengwa katika kuheshimiana. Mume na mke wanapaswa kuheshimiana na kuifanya jamii yao kuwa thabiti. Sual hilo hupambanua usawa wa Mwafrika. Mtazamo wa Tumaini unaoneshwa na mwandishi anaposema:

> “… unaelewa usawa labda kwa maana ya kizungu-maana ya kuamrishana na kujadiliana. Ubishani ndio mwanzo wa matata. Usawa wa Kiafrika ni usawa wa kuheshimiana. Tangu zamani wazazi wetu waliheshimiana. Hii ni dhahiri kabisa. Ndiyo maana walikaa pamoja…” (uk. 72).

Mtazamo wa Tumaini kwamba heshima ndiyo msingi wa usawa wa Kiafrika unajengwa na Ontolojia ya Kiafrika juu ya kuwapo kwa usawa na umuhimu wa kuheshimiana katika jamii. Aidha, imebainika kuwa kuwapo kwa mikinzano hiyo ya kimtazamo baina ya Tumaini na mama Resi kunabainisha falsafa ya Kiafrika juu ya kuheshimiana baina ya wanajamii. Falsafa hiyo imejengwa katika itikadi ya kani ambayo inajipambanua katika kuheshimiana, kuheshimu miiko na maadili ya jamii. Mtazamo wa Tumaini unabainisha kuwa kwa Waafrika haki na usawa havijengwi katika kujadiliana, kushiriki maamuzi na kusaidiana majukumu bali hujengwa katika misingi ya heshima, yaani kuheshimiana baina ya mwanamke na mwanamume. Kuchagiza hili, Ilomo (2017:47) anapofafanua mbinu ya

mazungumzo baina ya wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* anasema:

> Mwandishi ametumia mbinu ya kumpambanisha mhusika Tumaini na Mama Resi katika mazungumzo. Katika mazungumzo hayo ndipo tunapogundua mitazamo ya wahusika hawa kuhusu usawa kati ya mwanamume na mwanamke. Kupitia mazungumzo hayo msimulizi-mwandishi anawasawiri wahusika hawa kuwa ni watu waliokuwa wakitofautiana kimtazamo na kifikra. Wakati Tumaini anasawiriwa kama mtu aliyekuwa akiamini katika heshima; Mama Resi anasawiriwa kama mtu aliyekuwa akiamini katika haki na usawa wa kijinsia. Usawa huo anaouamini Mama Resi, kwa Tumaini ulikuwa ni usawa uliojikita katika mtazamo wa Kizungu wakati kwa mtazamo wa Kiafrika usawa ni wa kuheshimiana (uk. wa 72).

Kutokana na mazungumzo hayo, pia inaibuliwa dhamira ya Uafrika dhidi ya Umagharibi. Katika dhamira hii tunaelezwa kuwa kwa mtazamo wa Kiafrika heshima ni jambo la msingi wakati kwa mtazamo wa Kimagharibi usawa wa kijinsia ndilo jambo la msingi bila kujali usawa huo unazingatia utu.

`Nukuu hii inaonesha kuwa heshima ni nguzo muhimu inayompambanua Mwafrika na ndiyo msingi unaoijenga jamii thabiti. Heshima hii huanzia kwa kuwaheshimu wahenga, wazazi na jamii inayomzunguka (Chuachua, 2016). Hivyo, kuwapo kwa mikinzano ya kimtazamo juu ya suala la haki na usawa kumebainisha falsafa ya Kiafrika ambayo imejengwa katika imani kwamba maisha ya Mwafrika yanaongozwa na utu, heshima na kujaliana (Faustine, 2017). Kuheshimiana ni jambo muhimu kwa Mwafrika kuliko kupambania haki na usawa baina ya wanandoa. Mwafrika anaongozwa na imani kwamba utu wa mtu hutokana na namna anavyoheshimu kaida za jamii na si katika haki na usawa baina ya mwanamke na mwanamume (Mtega, 2023). Hivyo, utofauti wa kimtazamo baina ya wahusika umebainisha falsafa ya Kiafrika ya kuheshimiana kama msingi wa maadili, ndoa na jamii na sio haki na usawa wa kijinsia.

## 5.2 Uzazi

Uzazi ni kipengele kimojawapo kinachobainisha fikra, maarifa na mitazamo inayopambanua falsafa ya Waafrika juu ya maisha na namna wanavyoutazama na kuupa maana ulimwengu wao (Mbiti, 1975; Chuachua, 2016; Mpalanzi, 2018). Uzazi ni kipengele kimojawapo kinachoibua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Mikinzano ya kimtazamo kuhusu uzazi inajitokeza kupitia mazungumzo baina ya mhusika Tumaini, wazazi wa Leonila na wazazi wa Anastazia. Mazungumzo yalifanyika baada ya Tumaini kumpatia mimba Leonila na kuikataa. Kitendo cha Tumaini kukataa mimba mbele ya wazazi wa Leonila na kuwaambia kuwa mtoto akizaliwa apewe mbwa, kinapambanua mtazamo wake juu ya kutothamini uzazi. Mwandishi anaonesha hili anapoeleza kuwa:

> Kasala alitaka Tumaini amwoe Leonila kwa nguvu. Tumaini alipoitwa mkutanoni siku ya pili hakuwa na mengi ya kusema. Leonila alipoulizwa kama alikuwa tayari kuolewa na Tumaini alisema haraka: "Mimi lazima anioe! Amekwishaniharibu!" Tumaini alipoulizwa alijibu kwa kiburi. Mimi siwezi kumwoa Leonila, mimba si yangu. Hata kama akizaa, mtoto wake mnaweza kumtupia mbwa!"... Wazee walitingisha vichwa vyao kwa mshangao. "Wewe hukuzaliwa na mtu? Unaweza kwenda nyumbani!" (uk. 26).

Nukuu hii inaonesha mikinzano ya kimtazamo baina ya Tumaini na wazazi wa Leonila na Anastazia juu ya suala la uzazi. Majibu ya Tumaini kuhusu mimba ya Leonila yanadhihirisha mtazamo wake juu ya namna asivyothamini uzazi. Sambamba na hilo, mtazamo wa Tumaini wa kutothamini uzazi unajitokeza pia katika mazungumzo baina yake, Anastazia na Leonila walipokuwa Shinyanga. Mazungumzo haya yalikuwa baada ya Leonila kufika nyumbani kwa Tumaini kwa ajili ya kumkabidhi Tumaini mtoto wake. Mwandishi anatuonesha majibizano hayo kupitia wahusika kama ifuatavyo:

> Chukua mtoto wako ukae naye" Leonila alisema. "Hata! Mimi siwezi! Huyu nilisema zamani kwamba si mtoto wangu!" Wakati alipokuwa akisema maneno haya Leonila alikuwa amekwisha kwenda. Tumaini alimweka mtoto hapo nje. Mtoto alianguka chini, na sasa alikuwa amelala chali akitazama juu; mikono yake alikuwa ameisambaza… (uk. 88).

Nukuu hii inaonesha namna Tumaini alivyomkataa mtoto na kumuacha pale chini. Kitendo hicho kinapambanua wazi mtazamo wa Tumaini wa kutokuthamini uzazi wake. Mtazamo kama huo ni jambo baya kwa Mwafrika kwa sababu unakinzana na mitazamo inayopambanua falsafa ya Kiafrika. Mtazamo aliouonesha Tumaini juu uzao wake unakinzana na ule wa Anastazia ambaye anaamini kuwa ndani ya uzao wa mtoto huyo kuna vizazi vyao vingine vingi ambavyo vingekuja kuwashtaki juu ya matendo wanayoyafanya. Mtazamo wa Anastazia juu ya uzazi unabainishwa na mwandishi anapoeleza

> Haikuwa kitu kingine isipokuwa kizazi chetu ndicho kilikuwa kimeanguka. Mtoto alianza kulia. Ndani ya mtoto huyo mmoja. Anastazia aliwaona wajukuu wetu wa baadaye wakitushtaki mbele ya jua na ulimwengu wote. Ndani ya mtoto huyo aliona jinsi kizazi kimoja kinavyoweza hali ya maisha ya kizazi kingine…" Anastazi aliamka na kumbeba mtoto. Alimpangusa mchanga na kumwingiza ndani ya nyumba kabla majirani kukusanyika na kuuliza kulikuwa na nini? (uk. 89).

Nukuu hii inaonesha wazi mkinzano wa kimtazamo juu ya uzazi baina ya mhusika Tumaini na Anastazia. Kitendo cha Anastazia kuinuka na kumchukua mtoto huku akiamini kuwa ndani ya mtoto yule kuna maisha ya vizazi vyao vijavyo,

kinabainisha mtazamo wake juu ya namna anavyouthamini uzazi. Anastazia anaonesha hali ya kujali na kuingiwa na hofu juu ya namna anavyomtazama mtoto huyo na kuona wajukuu zao watakavyowashtaki mbele za jua na ulimwengu. Maneno ya Anastazia yanabainisha falsafa ya Kiafrika juu ya kuthamini uzazi. Anastazia anautazama uzazi kama bahati, baraka, na mwendelezo wa kuwapo kwa vizazi vingine katika ulimwengu. Mtazamo wa Anastazia juu ya uzazi unaongozwa na mawazo ya Ontolojia ya Kiafrika inayotazama uzazi kama baraka, bahati na mwendelezo wa kuwapo, na njia ya milele (Mukolozi, 2017). Hivyo, mtazamo wa Anastazia juu ya uzazi unabainisha falsafa ya Kiafrika ambayo imejengwa katika imani kwamba uzazi ni baraka, bahati, chanzo cha maisha, ukamilifu wa maisha, mwendelezo hai wa vizazi, kuwapo kwa maisha na ulimwengu (Alembi, 2001; Sengo, 2010; Mbiti, 2011; Mtega, 2023).

Kwa mantiki hiyo, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika juu ya suala la uzazi inabainisha maarifa na imani inayopambanua falsafa ya Kiafrika kwamba uzazi ndio chanzo cha kuwapo kwa maisha na ulimwengu. Uzazi ndio mwendelezo wa kuwapo na ndio unaokamilisha maana na dhana ya ulimwengu. Imani hii imejipambanua vyema kupitia mtazamo wa mhusika Anastazia ambaye anaamini kuwa ndani ya mtoto huyo mmoja kuna wajukuu ambao ni udhihirisho wa kuwapo kwa vizazi vingine vitakavyoendeleza kuwapo kwao.

### 5.3 Malezi

Dhana hii inarejelea uangalizi wa karibu wa wazazi kwa watoto kiroho, kimwili, kiafya, kiakili na kitabia (El-Maawy, 2011). Kwa muktadha wa Kiafrika suala la malezi limefumbatwa katika kuzifahamu mila, desturi, tamaduni na miiko ya jamii (Mbiti, 2011). Malezi ndio msingi unaotoa fursa ya kukamilishana na kupata mtu kamili. Malezi huanzia katika ngazi ya familia ambapo wazazi huwa na jukumu kubwa la kuwaangalia na kuwafundisha watoto maadili yanayofaa kisha jukumu hilo hufanywa na wanajamii wote (Alembi, 2001). Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, suala la malezi limejitokeza na kuonesha mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika ambayo inabainisha falsafa ya Kiafrika. Katika riwaya hii, suala la malezi linajitokeza kwa namna mbalimbali. Kuna malezi yasiyofaa anayopata Tumaini kutoka kwa wazazi wake. Pia, kuna malezi ya Leonila kutoka katika mikono ya baba mkali na mwenye kuwatunza binti zake kama mboni ya jicho na malezi ya bibi yake Leonila ambayo yanakuwa tofauti na baba yake Leonila.

Tumaini ni mtoto pekee anayebahatika kuishi baada ya wazazi wake kufiwa na watoto wao wawili wa mwanzo. Malezi ya Kapinga na Muyango kwa mtoto wao Tumaini yanamwandaa vibaya katika kukabiliana na maisha yake ya ukubwani hususani baada ya wazazi wake kufariki. Tumaini anadekezwa sana na wazazi wake, hata pale anapoonekana kufanya makosa harekebishwi. Mwandishi anafafanua kuhusu malezi ya Tumaini akisema:

> …kila alicholilia alipewa. Siku moja Tumaini alimchoma mlezi wake jichoni. Yule mvulana alimpiga Tumaini kidogo. Tumaini alikimbia kwenda kushtaki kwa mama yake. "Mama, mpishi amenipiga!" "Kwa nini umempiga mtoto wangu!" Muyango alifoka. "Alikuwa karibu kunichoma jichoni!" mlezi wake alijibu. "Kuna tofauti gani kati ya jicho lako na la ng'ombe! Usirudie tena kupiga mtoto wangu kwa jambo dogo kama hili!" Tangu alipoanza kuzungumza Tumaini alizuiliwa na mama yake kumwita mlezi wake kwa jina. "Sema mpishi!" (uk. 11).

Nukuu hii inaonesha namna malezi ya Tumaini yalivyoathiriwa na mtazamo wa Muyango, mama yake. Muyango alimpenda sana Tumaini na kumlea kwa kumdekeza, kutomuonya, kutomuadhibu wala kumfundisha heshima na maadili ya jamii. Mtazamo wa Muyango kimalezi unatofautiana na wa Kapinga mumewe. Kapinga alijali sana urithi wa Tumaini, hivyo, alihangaika kutafuta mali kwa lengo la kumrithisha mtoto wake baada ya kifo chake. Mwandishi anabainisha mitazamo ya Muyango na Kapinga juu ya malezi anaposema:

> Muyango alipokuwa akifanya kosa la kumpenda Tumaini kuzidi kiasi, Kapinga alifanya kosa la kujali sana Tumaini atarithi nini, pesa ni ya kupeleka benki ili watakapokufa mtoto wao apate pesa nyingi za kurithi. Wakati wao wa maisha walitumia kiasi kidogo sana cha pesa. Mara nyingi utamwona Muyango jioni na bakuli lake akizunguka katika mihogo ya watu akichuma majani ya mihogo (uk. 12).

Nukuu hii inaonesha namna mitazamo ya wazazi wa Tumaini ilivyoathiri maisha ya Tumaini kimakuzi, kitabia na kimwenendo. Malezi ya Muyango na Kapinga hayakumfundisha kijana wao maadili bora, miiko, heshima wala namna sahihi ya kuishi katika jamii. Kimsingi, Tumaini alilelewa katika misingi iliyokwepa na kukengeusha falsafa ya Kiafrika juu ya malezi. Hivyo, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuwapo kwa mikinzano ya kimtazamo baina ya malezi ya Tumaini kunabainisha falsafa ya Kiafrika kwamba maisha ya Mwafrika yamefungwa katika itikadi ya kani ambayo huhusisha falsafa ya heshima na kuheshimiana, kuheshimu miiko na maadili ya jamii (Mulokozi, 2017). Sambamba na hilo, tunaona namna mitazamo ya Kapinga na Muyango ilivyoathiri malezi ya Tumaini kitabia, kimaamuzi na kiakili. Athari ambazo zimechochea kuwapo kwa mikinzano na mivutano baina ya Tumaini na jamii inayomzunguka. Mikinzano hiyo imetusaida kubainisha falsafa ya Kiafrika ambayo imejengwa katika imani kwamba jukumu la malezi ya mtoto huanza kwa mzazi kisha jamii inayomzunguka (Mtega, 2023). Kuchagiza hilo, methali kama 'mtoto umleavyo ndivyo akuavyo' na 'asiyefunzwa na mamaye huhunzwa na ulimwengu' zinakusudia kupambanua falsafa kwamba malezi ya mtoto huanzia kwa mzazi kisha jamii inayomzunguka.

Mikinzano ya kimtazamo juu ya malezi inajitokeza pia kupitia malezi aliyopata Leonila kutoka kwa Kasala na Mungere ambao ni wazazi wake na yale aliyoyapata kwa bibi yake aitwaye Mugala. Kasala alizingatia maadili ya jamii

katika malezi na alikuwa mkali katika malezi ya watoto wake. Kasala hakutaka mtu yeyote awe na mazoea ya kufika katika mazingira ya nyumba yake akiamini kuwa hiyo ndiyo njia sahihi ya kuwalinda mabinti zake dhidi ya watu wenye nia mbaya. Ukali wa Kasala ulimjengea hofu zaidi mke wake Mungere baada ya kugundua kuwa Leonila amepata mimba. Mwandishi anaeleza haya Mungere anaposema:

> Leonila, baba yako atakuwa mkali kama simba aliyepigwa mkuki mguuni. Hakika, jambo ulilotenda si la busara. Baba yako atakurarua vipande vipande. Leonila, tafadhali nieleze mambo haya yote yamekwendaje na ni nani aliyeyatenda. Leonila alimtazama dada yake usoni akionyesha alama za kutafuta msaada (uk. 6).

Nukuu inaonesha kuwa ukali wa Kasala, ulimsukuma Leonila kumtaja aliyempa mimba kuwa ni Tumaini, na kwamba mimba hiyo aliipata alipokuwa anatoka kisimani kuchota maji. Hata hivyo, si kweli kwamba Leonila alipata mimba hiyo alipokuwa anatoka kisimani, bali aliipata baada ya bibi yake kumfanyia mpango wa kuhusiana na Tumaini kimapenzi, wazazi wa binti huyo walipokuwa Shinyanga kwa mtoto wao wa kiume aitwaye Denis. Tangu wakati huo, Leonila na Tumaini waliendelea na mahusiano yao bila wazazi wake Leonila kujua.

Imebainika kuwa mtazamo wa Kasala juu ya malezi ya binti zake unakinzana na Mugala, bibi yao, ambaye ni mama yake Kasala. Mugala alikuwa na malezi mabaya kwa wajukuu wake na hata kuamua kumfanyia mpango Tumaini kumpata Leonila baada ya kuomba kupewa ugolo na Tumaini kutimiza hitaji hilo kwa Mugala. Mwandishi anaeleza haya kupitia majibizano baina ya Tumaini na Mugala kama ifuatavyo::

> "Mama mimi nimekuja kutafuta msaada wako."
> Msaada wa kufanya nini?"
> "Nimejaribu kumpata Leonila lakini nimeshindwa. Baba yake mkali na yeye mwenyewe hatoki nje mara nyingi."…
> "Mama huwezi kunisaidia katika jambo nililokwambia?"
> " Kama unataka msaada wangu niletee ugolo kesho halafu nitakufanyiza mpango". Tunalala nao nyumba moja; nyumba hiyo," aliionesha kwa mdomo…
> Leonila alikuwa amekwisha vaa khanga zake kwa safari ya usiku. Hivyo ndivyo Tumaini alivyoanza uhusiano wake na Leonila (kur. 18 na19).

Nukuu hii inadhihirisha mtazamo wa Mugala wa kwamba kuwa Kasala anawanyima uhuru wajukuu zake. Hivyo, Mugala alitumia nafasi ya kukaa chumba kimoja na wajukuu zake kama fursa ya kuwapa uhuru waliouhitaji, mbinu za kutoroka usiku na yeye kujipatia ugolo pasipo Kasala na mkewe kufahamu. Mtazamo wa Mugala juu ya malezi uliathiri maisha ya wajukuu zake. Tofauti za

kimtazamo juu ya malezi baina ya Kasala na Mugala zinasimuliwa na mwandishi kama ifuatavyo:

> Usiku Kasala alikuwa bado na hasira. Alikuwa amekwisha sikia hadithi yote ya Tumaini. Alikwenda kumfokea mama yake. “Kwa nini unaniharibia binti zangu” Unakubali kudanganywa kwa ugolo! Lini uliomba ugolo nikakunyima!” Mugala alikataa kula…(uk. 22).

Nukuu hii inadhihirisha kuwa mikinzano ya kimtazamo juu ya malezi baina ya Mugala na Kasala imeleta athari katika makuzi, malezi na mienendo ya Leonila. Hivyo, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa mikinzano ya kimtazamo juu ya malezi inayojipambanua kupitia Muyango na Kapinga kwa Tumaini na mzee Kasala na Mugala kwa Leonila inaibua falsafa ya Kiafrika inayojipambanua kupitia imani kwamba kwa Mwafrika jukumu la malezi ya mtoto huanzia kwa wazazi kisha jamii nzima inayomzunguka (Alembi, 2001). Wazazi ndio mhimili kwa kwanza katika kuwafunza watoto wao maadili, tamaduni na miiko ya jamii kisha jamii ndipo hupata nafasi ya kuwaonya, kuwakumbusha na kuwafundisha wanajamii maadili na misingi ya jamii (Samwel, 2015; na Mulokozi, 2017). Aidha, Sengo (2008) anasema kwamba mafunzo ya awali yanayotolewa na mafundi wa Kiafrika yana maana na thamani kubwa. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga kumfundisha mtoto miiko ya Kiafrika na uadilifu kulingana na misingi ya jamii. Hivyo, mzazi ambaye hushindwa kumkanya, kumfundisha na kumlea mtoto wake kulingana na miiko na maadili ya jamii, hukiuka mila, desturi, tamaduni na falsafa ya maana yake, Kiafrika juu ya malezi. Falsafa ya Kiafrika juu ya malezi imejengwa katika msingi ya itikadi ya kani ambayo huhusisha falsafa ya heshima, kuheshimu miiko ya jamii na maadili.

### 5.4 Utamaduni

Katika kufafanua dhana ya utamaduni, Wizara ya Elimu na Utamaduni (1999) katika *Sera ya Utamaduni* inaeleza kuwa utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha na jamii nyingine. Utamaduni ndicho kitambulisho kikuu cha taifa na kielelezo cha utashi na uhai wa watu wake. Halikadhalika, utamaduni una nguzo muhimu ambazo ni lugha, mila na desturi, chakula, mavazi, historia pamoja na michezo. Utamaduni ni kipengele kimojawapo kinachojitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na kupambanua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika ambayo inabainisha falsafa ya Kiafrika. Mikinzano baina ya wahusika juu ya utamaduni inajitokeza katika suala la mavazi hususani anayopaswa kuvaa mwanamke. Mwandishi anaonesha mpambano wa kimawazo na kimtazamo juu ya mavazi baina ya Tumaini, Dennis na mama Resi anaposema:

> Hivi wewe unaonaje juu ya suala hili la nguo?” Mama Resi aliuliza. “Juu ya suala hili sina mengi ya kusema juu ya wavulana; isipokuwa ninayo mengi kuhusu wanawake. Nionavyo mimi kuna mambo mawili

> yanayopingana katika suala hili uhuru wa wanawake na utamaduni. Haya ndiyo mambo mawili yanayopingana. Wale wanawake waliosoma wamekwisha sikia neno 'uhuru wa wanawake' wakitaka kuanzisha mtindo wao wa kuvaa na kufunga vitambaa, hawana haja ya kuwauliza waume kwanza. Upande mwingine utaona wazo hili linapingana na utamaduni wetu. Utamaduni wetu ni tofauti na ule wa Kizungu. Jambo la uhuru wa mwanamke au usawa kati ya mume na mke linafaa sana watu kama hao... (uk. 79).

Nukuu inaonesha namna Tumaini anavyopambanua mtazamo wa Kiafrika na kuutofautisha na ule wa Kizungu juu ya mavazi hususani anayopaswa kuvaa mwanamke. Tumaini anaamini kuwa suala la uvaaji limefungwa katika mambo mawili, yaani 'uhuru wa mwanamke' na 'kuwapo kwa utamaduni'. Anaamini kuwa wanawake waliosoma wanavaa mavazi yanayokiuka utamaduni wa Kiafrika. Wanawake hao wasomi wamejifunza kuhusu uhuru wa mwanamke na wanautumia uhuru walioupata kukiusha miiko ya jamii kwa kutokuwauliza wanaume wao juu ya aina ya mavazi wanayopaswa kuvaa wao kama wanawake. Mtazamo wa Tumaini unaongozwa na mawazo ya Kiontolojia ya Kiafrika ambayo yanajikita katika kujiheshimu, kujisitiri na kutunza utu. Mtazamo wa Kiafrika juu ya utamaduni wa uvaaji unajitokeza pia kupitia mhusika Dennis.

Denis anapambanua mtazamo wake kwamba wanawake wanaovaa mavazi kama taiti na suruali wanatawaliwa na mawazo ya watu wengine. Hii ina maana kuwa Dennis anawatazama kama watu wasioishi uasilia wao bali wanaomithilisha uhalisia wa watu wengine. Mwandishi anabainisha haya anaposema:

> Wewe huoni kwamba wanawake wanaovaa taiti na suruali wanakataa hali yao na kuchukua ya watu wengine? Huoni kwamba wanatawaliwa na mawazo ya watu wengine? Denis alisema… (uk. 79).

Kupiti nukuu hizo tumebaini kuwa mtazamo wa Tumaini na Denis unajengwa na kuwapo kwa athari za Umagharibi katika utamaduni wa uvaaji kwa Waafrika. Dennis anaona kuwa kuvaa mavazi kwa mitindo ya Kimagharibi ni kutawaliwa kifikra na kuukana utamaduni wa Kiafrika. Mtazamo wa Dennis na Tumaini umefungwa katika misingi ya utamaduni wa Mwafrika wa kwamba mwanamke anapaswa kuongozwa na misingi na maadili ya Mwafrika hususani katika mavazi. Utamaduni wa Kiafrika unaongozwa na maadili ambayo yanamtaka mtu kujiheshimu, kujisitiri, kuuheshimu mwili wake na kuutunza (Bitek, 1989).

Mtazamo wa Tumaini na Denis juu ya uvaaji na kujisitiri kwa kuzingatia maadili ya Kiafrika unakinzana wa mama Resi ambaye anaupigia chapuo utamaduni wa Kimagharibi juu ya uvaaji na kuona kuwa hauna athari zozote kwa sababu tamaduni huingiliana na kuathiriana. Mwandishi anaonesha mtazamo wa mama Resi anaposema:

> Mama Resi anajibu hoja za Tumaini kama zilivyoelezwa katika gazeti kwamba "Ubaya wetu siku hizi, tunajaribu kuchukia kila kitu

> kilichoachwa nyuma na Mzungu. Tangu uhuru, watu wengi wanafikiri kwamba kila kilicho cha Mzungu ni cha kikoloni. Kuna mambo mengi ya Mzungu ambayo ni sheria na sharti yazingatiwe. Hakuna nchi ambayo ina utamaduni wake wa pekee siku hizi: kwa sababu njia za kusafiri siku hizi zimerahisishwa. Utamaduni huvutana, hushawishana, kuingiliana na utamaduni wa nchi mbalimbali. Utamaduni ni mchanganyiko. Tukitaka kuwa na utamaduni wetu pekee, basi tusiwe na uhusiano wowote na nchi za nje… (uk. 76).

Nukuu hii inabainisha mtazamo wa mama Resi juu ya uvaaji. Mama Resi anaamini kuwa kitendo cha Mwafrika kuvaa pasipo kujisitiri ni jambo la kawaida ambalo limetokana na athari za mwingiliano wa tamaduni. Mtazamo wa mama Resi unaonesha kuwa Umagharibi una nafasi katika maisha ya Mwafrika, jambo ambalo linapingwa na Tumaini pamoja na Dennis ambao wanaonesha mitazamo yake kwamba misingi ya Kiafrika hususani suala la mavazi linapaswa kuzingatia. Mwafrika anapaswa kuvaa mavazi yanayomsitiri na kutunza utu wake. Suala la kuwapo kwa mikinzano ya kimtazamo juu ya utamaduni wa mavazi na uvaaji, linaibua mawazo na maarifa yanayopambanua falsafa ya Kiafrika kwamba Mwafrika anaamini katika kujisitiri kimavazi kama njia mojawapo ya kutunza utu, haiba na heshima na maadili ya Mwafrika (Bitek, 1989; Omoregbe, 1998). Hivyo, kupitia mjadala uliofanyika imebainika kuwa utamaduni wa uvaaji kwa Mwafrika ni mojawapo ya mambo yanayopambanua falsafa ya itikadi ya kani katika jamii. Itikadi ambayo imejengwa katika kuheshimu maadili ya jamii. Uvaaji ni sehemu mojawapo ya maadili ya Mwafrika na jambo linalopaswa kuzingatia maadili na mila za Kiafrika.

### 5.5 Ujamaa

Ujamaa ni dhana iliyotokana na neno jamaa au jamii. Inahusu mfumo mzima wa maisha, taratibu, mila na desturi, kanuni, misingi, miiko na taswira nzima ya utamaduni wa maisha baina ya jamaa katika jamii husika (Rogers, 2021). Pamoja na kuwapo kwa tofauti nyingi za kimila, desturi na lugha baina ya makabila 120 yaliyopo Tanzania, kitu kimoja kilichokuwapo ndani ya kila kabila ni utamaduni wa maisha ya kijamaa. Ujamaa wa Kitanzania na Kiafrika ni sehemu ya utamaduni hai na asilia. Aidha, TUKI (2004) wanatoa fasili mbili kwanza ujamaa ni udugu. Pili, ujamaa ni mfumo wa kiuchumi, kijamii au kisiasa unaowezesha umma kumiliki njia kuu za kuzalisha mali na mgawanyo hai wa mapato ulioasisiwa na aliyekuwa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu J.K. Nyerere. Mtazamo wa pili unapingwa na (Rogers, 2021) anapoeleza kuwa dhana ya ujamaa baada ya kutangazwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1967 katika Azimio la Arusha ilifananishwa na kubebeshwa sura mpya yenye mfumo wa Kisoshalisti. Dhana ya ujamaa ilionekana mpya katika jamii, jambo ambalo si sahihi kwa sababu tangu enzi za mababu mfumo wa maisha wa Waafrika ulijengwa katika itikadi ya kijamaa, yaani watu waliishi kijamaa na kila jambo lilifanyika kwa masilahi ya

jamii na umma. Suala la ujamaa linajitokeza katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na kuibua mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika. Mwandishi anawatumia wahusika wake kupambanua maarifa na mitazamo juu ya kuwapo kwa ujamaa wa aina mbili, yaani ujamaa wa Kiafrika na ujamaa wa Kimagharibi.

Tunaona mkinzano wa kimtazamo juu ya suala la Ujamaa unaanza kujitokeza wakati Mkuu wa Wilaya anafanya kikao chake cha kisiasa katika mji wa Shinyanga. Wakazi wa Shinyanga wakiwamo wazee waliweka wazi mitazamo yao juu ya Ujamaa wa kigeni kwa kuuliza maswali ambayo yalionesha wazi juu ya misimamo ya kijamaa kwa misingi ya Kiafrika. Haya yanajitokeza kupitia maswali ya wahusika kama ifuatavyo: mwandishi anaposema:

> Swali langu ni hili: zamani tulikuwa tukiishi vizuri na jirani zetu. Huyu asipokuwa na mboga anakwenda kuchukua kwa fulani. Huyu akiuguliwa majirani wanafika. Sasa nasikia hakuna cha bure. Sijui. Sisi tulikuwa tukiishi vizuri bila fujo. Leo tunaambiwa sijui dunia uwanja wa fujo; na sisi wazee hatutaki fujo. Sasa sijui fujo itatufikisha wapi...
>
> Wakoloni walituletea zao la pamba. Sisi tukawa tunalima ili kulisha viwanda vyao huko Ulaya kwa bei wanayotupangia. Walifungua mabenki na makampuni, na mirija ya aina nyingi. Mambo haya sasa yamo mikononi mwa umma. Mabasi yetu, mabenki yetu, majumba yetu. Huu ndiyo Ujamaa. Ingawa siasa yetu inajali sana utu. Kiuchumi hatuwezi kukaa kama watakatifu. La sivyo, mataifa makubwa yatatuonea daima. Kwa hiyo, tunafanya fujo kidogo. Makampuni tunachukua, mabenki tunachukua tunaiweka mikononi mwetu, Na huko vijijini tunajiunga pamoja ili kuharakisha maendeleo yetu (uk. 118).

Nukuu hii inaonesha mkinzano wa kimtazano baina ya wananchi na Mkuu wa Wilaya. Wananchi wanaamini kwamba Ujamaa wa Kiafrika umejengwa katika kufanya kazi, kusaidiana katika kila hali na kushirikishana masuala mbalimbali ya kijamii kwa masilahi ya jamii nzima. Mtazamo wa wananchi unaongozwa na Ontolojia ya Kiafrika ambayo imejengwa katika itikadi na imani katika umoja na ushirikiano, mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo na kuthamini kazi. Kupitia misingi ya Ontolojia ya Kiafrika, ni dhahiri kuwa mtazamo wa wananchi unakinzana na ule unaofafanuliwa na Mkuu wa Wilaya juu ya Ujamaa mpya ambao haukuwapo na si asili ya misingi ya Kiafrika. Ujamaa huo mpya unaegemea katika upande mmoja wa wananchi kwa kuwataka wahamie katika vijiji vya Ujamaa na kusalimisha mali, mashamba na mifugo waliyonayo kwa masilahi ya umma.

Mwandishi anaonesha kuwa Ujamaa huu ni wa kibaguzi na kinyonyaji kwa sababu unawapa viongozi uhuru wa kuishi mijini, kutumia magari na kutochangamana na wananchi katika vijiji vya Ujamaa. Jambo hili ndilo linalopingwa na wananchi wa Shinyanga kama lilivyosimuliwa na mwandishi (taz. uk. 118). Hivyo, tunaona kuwa kuingia kwa aina mpya ya Ujamaa katika jamii

kulisaidia kupambanua fikra, imani na mitazamo ya Waafrika juu namna wanavyouelewa na kuuishi ujamaa wao asilia. Wananchi wanapinga mfumo mpya wa kinyonyaji kwa kueleza namna wasivyoafiki mitazamo mipya juu ya aina mpya ya unyonyaji inayotambulishwa kuwa ni Ujamaa. Kuwapo kwa mkinzano wa kimtazamo baina ya wananchi wa Shinyanga na Mkuu wa Wilaya kunabainisha wazi misingi ya Ujamaa wa Kiafrika. Misingi hiyo inabainisha falsafa ya Kiafrika ya kuthamini kazi, umoja na ushirikiano pamoja na kuimarisha mshikamano na ukamilishano wa maumbile na vilivyomo (Mulokozi, 2017). Maana ya falsafa hiyo ndiyo msingi unaowaunganisha Waafrika.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imemakinikia mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika inavyoweza kubainisha falsafa ya Kiafrika. Mjadala umeongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* imejitokeza katika kipengele cha ndoa, uzazi, malezi, utamaduni na Ujamaa. Wahusika wamevishwa uhusika unaobeba mitazamo yao juu ya vipengele hivyo huku wakionesha namna wanavyokinzana kimtazamo. Mikinzano hiyo ya kimtazamo imesaidia kubainisha imani, itikadi na maarifa yanayoipambanua falsafa ya Kiafrika. Imebainika kuwa mitazamo ya Mwafrika hufungamanishwa na malezi na makuzi aliyoyapata mtu, imani, itikadi na maarifa yanayofungamana na jamii yake. Mambo hayo hutambulisha, huelezea na kutofautisha mitazamo ya mhusika moja na mwingine. Vilevile, makala hii imeonesha namna mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika inavyoibainisha falsafa ya Kiafrika. Imebainika kuwa maisha ya Mwafrika yamejengwa katika falsafa ya kuthamini uzazi kama mhimili wa kuwapo na mwendelezo hai wa vizazi, malezi bora yanavyopaswa kufungamana na maadili ya jamii huku heshima ikiwa ndiyo msingi wa haki na usawa kwa Kiafrika. Pia, imebainika kuwa maisha ya Mwafrika yanaongozwa na falsafa ya kuwapo kwa umoja na ushirikiano, kuheshimiana, kuthamini kazi na kuthamini maadili ya jamii. Mjadala uliofanyika umedhihirisha kuwa mikinzano ya kimtazamo baina ya wahusika katika riwaya teule hubainisha falsafa ya Kiafrika.

## Marejeleo

Alembi, E. (2001). The Construction of the Abanyole Perception on Death Through Oral Funeral Poetry. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi.

katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Diegner, L. (2005). “Intertextuality in the Contemporary Swahili Novel: Euphrase Kezilahabi’s *Nagona* and Wilium E. Mkufya’s *Ziraili* na *Zirani*. *Swahili Forum*. 12: 25-35.

Faustine, S. (2017). Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ilomo, L.F. (2017). Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa zao: Uhakiki wa Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ya E. Kezilahabi. *Mulika*. 34: 38-50.

Kagame, A. (1956). *The Rwandeese Bantu Philosophy of Being*. Brussels: Johnson Reprint Corperation.

Kajosi, S. (2013). Suala la Uzazi katika Ontolojia ya Kibantu na jinsi Ilivyojitokeza katika Riwaya za Kiswahili.” Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Saalam.

Kezilahabi, E. (2007). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi: Vide-Muwa publishers Limited.

Makumba, M.M. (2005). *Introduction to Philosophy*. Nairobi: Paulines Publications.

Mbiti, J. (1975). *Introduction to African Religion*. London: Heinemann.

__________ (1990). *African Religions & Philosophy*. London: Heinemann.

_________ (2011a). *Introduction to African Religion*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mihanjo, A. (2007). *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa: Toka Uyunani Hadi Afrika.* Morogoro: Salvatorian.

_______(2006). *Falsafa na Usanifu wa Hoja-Kutoka Wayunani hadi Watanzania (Waafrika).* Morogoro: Salvatorian.

Mkabarah, R.J. (1975). *Mwanamuziki wa Tanzania Salum Abdallah.* Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S.A.K. (1991). “Point of View as Stylistics Device in Kiswahili Novels.” *Kiswahili*. 58: 54-61.

Mpalanzi, L. (2018). “Mpaka kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili”. *Mulika*. 37: 131-150.

Mtega, W.S. (2023). Uchimuzi wa Kosmolojia katika Tambiko: Uchunguzi katika Ushairi wa Matambiko ya Wapangwa. Tasinifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1983). “*Dunia Uwanja wa Fujo* (Mapitio ya Kitabu).”*Kiswahili*. 50(1):1-12.

________(2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Omoregbe, J.I. (1998). “African Philosophy: Yesterday and Today,” Eze E.C (Mh.), *African Philosophy: An Anthology*. Cambridge: Blackwell Publishers. Kur 5-11.

P' Bitek, O. (1989). *Song of Lawino and Song of Ocol*. Nairobi: East Africa Education Publishing House.
Prince, G. (1982). *Narratology: The Form and Functioning of Narrative*. Berlin: Mouton Publishers.
Rimmon-Kenan, S. (1983). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Routledge.
Roberts, E.V. (1995). *Writing about Literature*. New Jersey: Prentice Hall, Inc.
Rogers, M. (2021). ‘‘Ujamaa ni utamaduni wa Watanzania, si itikadi ya kisiasa’’. *Mwananchi*. 21 Februari 2024. Uk. 7.
Senkoro, F.E.M.K. (1983). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
__________ (2011). *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam: KAUTTU.
Simpson, P. (1983). *Language, Ideology and Point of View*. London: Routledge.
Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.
TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la pili). Nairobi: Oxford University Press.
Uspensky, B. (1973). *A Poetics of Composition*. California: University of Califonia.
Wafula, R. (2002). “Language and Politics in East Africa Swahili Prose: Intextuality in Kezilahabi’s *Dunia Uwanja wa Fujo* ‘The World a Playground of Chaos,” katika S.G. Obeng and B. Hartford (Wah.), *Surviving Through Obliqueness: Language of Politics in Emerging Democracies.* New York: Nova Science Publishers inc. Kur. 19-29.
Wamitila, K.W. (1997). “Contemptus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi‘s Works.” *Kiswahili*. 60: 15-24.
Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
Wa Thiong’o, N. (1996). *Decolonizing the Mind*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
Wizara ya Elimu na Utamaduni (1999). *Sera ya Utamaduni.* Dar es Salaam: WEU.